*Mulika, Na. 41 (1), 65-78*
*Jarida la Taasisi ya Taaluma za Kiswahili*
*Chuo Kikuu cha Dar es Salaam*

# Nafasi ya Fasihi Simulizi katika Karne ya 21: Tathmini ya Nyimbo za Jando za Jamii ya Wakamba

Naomi Nzilani Musembi
Chuo Kikuu cha Sayansi na Tekinolojia cha Jaramogi Oginga Oginga
&
Toboso Mahero
Chuo Kikuu Kishiriki cha Alupe

DOI: https://doi.org/10.56279/mulika.na41t1.5

**Ikisiri**

Fasihi simulizi ni fani hai inayotekeleza majukumu muhimu katika karne ya 21. Kama ukumbusho wa maadili ya watu, fasihi simulizi hutoa mwonoulimwengu wa jamii na kutokana nayo, hali ya maisha ya kila siku huendelezwa. Wanajamii hueleza hali yao ya maisha, utamaduni wao, maoni, mitazamo, imani na mila zao kupitia kwa utanzu huu hasa kipera cha nyimbo. Katika jamii ya Wakamba, fasihi simulizi inatumika kuelezea mielekeo na falsafa kuhusu maisha ya wanajamii. Nyimbo ni mojawapo ya fani hai ya fasihi simulizi na hubadilika kadiri hali ya maisha inavyobadilika. Mabadiliko yanayoikumba jamii kwa njia moja au nyingine hujidhihirisha katika fasihi. Maadili yalikuzwa na hata sasa yanakuzwa kupitia nyimbo hasa za jando katika jamii ya Wakamba. Katika karne hii ya 21, jamii inakumbwa na matatizo mengi hususani magonjwa yasiyo na tiba, uraibu wa dawa za kulevya, ukosefu wa kazi kwa vijana , uabudu shetani, vita vya wenyewe kwa wenyewe miongoni mwa matatizo mengine. Ili kupambana na changamoto hizi, ni muhimu kuwa na nyenzo za mawasiliano zinazoweza kutumiwa kuwafahamisha wanajamii jinsi ya kukabiliana nazo. Nyimbo za jando ni miongoni mwa njia hizi kwani kupitia kwazo, ujumbe unaweza kuwasilishwa vyema zaidi kuhusiana na namna ya kukabiliana na matatizo hayo. Hivyo basi, lengo la makala haya ni kuonesha kuwa, fasihi simulizi hasa nyimbo za jando bado zina dhima muhimu katika jamii inayobadilika.

## 1.0 Utangulizi

Fasihi simulizi ni utanzu muhimu wa fasihi katika jamii kwani utamaduni wa jamii inayohusika hujidhihirisha kupitia utanzu huu (Wamitila, 2003). Dhima za fasihi simulizi ni anuwai. Mojawapo ya dhima hizi ni kuendeleza na kudumisha historia na utamaduni wa jamii husika. Tanzu za fasihi simulizi ni nyingi na kila utanzu una dhima yake kwa kila jamii yenye kumiliki fasihi hiyo. Nyimbo ni mojawapo ya tanzu hizo na umuhimu wake kwa jamii za Kiafrika ni bayana. Katika jamii za Kiafrika za kale, nyimbo hizi zilitekeleza majukumu mengi. Mathalani, Finnegan (1970) anasema kuwa katika maisha ya jamii za Kiafrika, nyimbo za kitamaduni zilikuwa na majukumu kadhaa muhimu. Anasisitiza kwamba Waafrika walikuwa na nyimbo ambazo ziliambatana na matendo anuwai yaliyo msingi kwa maisha yao. Takribani

jamii zote za Waafrika zilikuwa na nyimbo ambazo maudhui yake yalilenga ushindi wa vita, kuzaliwa, kupashwa tohara, harusi, maombolezi, kilimo, kulisha mifugo, kumlea mwana, na takribani shughuli zote za binadamu (King'ei, 1982). Japo ulimwengu umebadilika sasa, jamii nyingi za Kiafrika zingali zinaendeleza nyimbo za kitamaduni za kifasihi katika njia nyingi ikiwamo sherehe, maombolezi na matambiko. Katika jamii zinazoendeleza fasihi hii, nyimbo zake zina maudhui na mitindo inayohusiana na shughuli zinazotekelezwa wakati huo. Hata hivyo, maudhui na mitindo katika tanzu anuwai za fasihi simulizi hubadilika kulingana na wakati na husawiri historia na mwelekeo wa jamii (Nandwa na Bukenya, 1983).

Fasihi simulizi ya kila jamii huibuka na kujengeka katika hali halisi ya maisha ya kila siku. Kwa mujibu wa Simiyu (2007), nyimbo, kama utanzu wa fasihi simulizi, huendelea kupitia mabadiliko ya kijamii kadiri jamii inavyoendelea kubadilika. Fasihi simulizi ya kila jamii huweza kuathiriwa na mabadiliko yanayotokea kila wakati, ambayo hutokana na uhamiaji, maingiliano na mahusiano ya kijamii, kikabila, kidini, kisiasa au kiuchumi.

Suala la maudhui ya nyimbo limezungumziwa na wataalamu anuwai wakiwamo Nandwa na Bukenya (1983), Kavyu (1980), Somba (2000), na Watuma (2001). Mathalani, Nandwa na Bukenya (1983) wanadai kwamba kazi yoyote ya fasihi haiibuki katika ombwe bali hujikita katika maudhui yanayotokana na jamii. Hii inasisitiza hali kwamba kadiri hali ya maisha katika jamii inavyobadilika, ndivyo fasihi simulizi pia inavyobadilika. Mabadiliko haya hudhihirika katika nyimbo kwa sababu nyimbo ni kipera kimojawapo cha fasihi simulizi ambacho ni pendwa na ni msingi wa fasihi simulizi ya jamii za jadi na za kisasa.

Tafiti anuwai zimeonesha kwamba, tohara katika jamii ya Wakamba zilianza zamani na ziliambatanishwa na nyimbo katika awamu mbalimbali (Kingei, 1982; Nzioki, 1982; Kavyu, 1980; Somba, 2000; Watuma, 2001; Wathome, 2009). Msimu wa tohara ni wakati muhimu wa kuwatayarisha vijana ili kuchukua wajibu wa uhalisia wa maisha ya utu uzima. Huu huwa wakati wa kufungamanisha vijana na utamaduni wa jamii yao. Vijana hufundishwa kuhusu utamaduni na maadili ambayo yanakubalika katika jamii yao ya Wakamba. Aidha, sherehe ya tohara huwa mojawapo ya mifumo ya kuunganisha jamii yote ya Wakamba. Kwa mujibu wa Kimilu (1962), nyimbo za tohara katika jamii ya Wakamba huwezesha vijana kuwa na maadili, licha ya kuwatoa kutoka ujana kwenda utu uzima. Kavyu (1980) anaeleza kuwa watahiriwa wanapaswa kupitia tohara ili wawe wanajamii kamili. Tohara, kwa mujibu wa Somba (2000), hufanyika kati ya mwezi wa Juni na Septemba kila mwaka kwa sababu huu ni wakati wa kiangazi katika sehemu ya Ukambani. Kwa mujibu wa King'ei (1982), Wakamba huamini kwamba wakati wa kiangazi ndio mwafaka kwa sherehe za jando kwani vijana hupona haraka wakati wa jua kali kuliko wakati wa mvua.

## 2.0 Mbinu za Utafiti

Utafiti huu ulifanyika uwandani ili kupata data kuhusu nyimbo za jando za Wakamba za vipindi mbalimbali vya kihistoria. Utafiti ulifanywa katika kata sita za Nzyiitu, Kalimbui, Ngalange, Mwangea, Nzanzeni na Kaluilaa katika Kaunti ndogo ya Tseikuru, Kaunti ya Kitui. Vituo vya utafiti viliteuliwa kimakusudi. Mbinu za hojaji, mahojiano, na uchunguzi shiriki zilitumiwa kukusanya data. Utafiti ulihusisha kunakili na kurekodi majibu yaliyotokana na usaili wa ana kwa ana baina ya mtafiti na wasailiwa. Nyimbo za tohara zilizoimbwa katika kipindi cha kabla ya ukoloni zilipatikana kupitia mbinu ya mahojiano ya ana kwa ana na wahojiwa. Wahojiwa kumi na wawili waliokuwa na miaka kati ya 25 na 70 walishirikishwa. Tuliteua wahojiwa wenye miaka tofauti kwa kuwa nyimbo za tohara hubadilika kiwakati. Wahojiwa hawa waliteuliwa kimakusudi ili kupata wale walioshiriki katika jando ya Wakamba na wanaofahamu nyimbo zilizohusika. Tulizuru kila mhojiwa ili kurekodi nyimbo zilizohitajika katika utafiti huu. Baadaye, mjadala wa makundi ulitumiwa ili kuthibitisha nyimbo zilizorekodiwa. Data iliyokusanywa ilirekodiwa kwa kinasasauti, kusimbwa na kuchanganuliwa.

## 3.0 Nadharia ya Utafiti

Nadharia ya Ethnografia ya Mawasiliano ya Hymes (1974) ndiyo iliyotumika katika utafiti huu. Nadharia hii inahusu mtazamo wa isimu-jamii unaojikita katika vipengele vikuu vitatu vya muktadha, utamaduni, na mazingira mbalimbali katika jamii ili kuainisha lugha na matumizi yake. Mtazamo huu huchunguza namna tukio fulani katika jamii linavyoibua matumizi maalumu ya lugha ili kufanikisha malengo yaliyokusudiwa. Aidha, huchunguza jinsi wahusika wa lugha fulani wanavyoitumia lugha hiyo kwa kutekeleza majukumu yao ikiwa ni pamoja na kushauri, kuonya, kutia moyo, kukashifu, kubembeleza, kuliwaza, kukejeli tabia mbovu, kuelezea hisia mbalimbali, kuhifadhi utamaduni, kuwasiliana na hata kuburudisha. Mintarafu ya Hymes (1974) na Ngara (1982), mawasiliano huwepo na kukamilika miongoni mwa wanajamii kwa kuzingatia vigezo vya muktadha, hadhira lengwa, utamaduni na lugha ya jamii ambavyo ndivyo mihimili ya Nadharia ya Ethnografia ya Mawasiliano.

Mihimili hii ilitumika katika utafiti kuchunguza na kufafanua watumiaji lugha, na namna wanavyoitumia lugha katika utunzi wa nyimbo za jando ili kupitisha ujumbe unaokusudiwa kupitia maudhui.

## 4.0 Dhima ya Nyimbo za Jando za Wakamba katika Karne ya Ishirini na Moja

Fasihi nzuri ni ile yenye kuelimisha, kuhimiza, kuboresha au kuimarisha ujenzi wa jamii imara yenye uadilifu na usawa (Njogu, 2007). Njogu (1987) anaeleza kuwa maudhui ya fasihi yoyote ile huzalika kutokana na jinsi jamii ilivyo wakati huo. Wimbo una uwezo wa kutumiwa na jamii kama chombo cha kukosoa au kuongoza watu katika jamii husika. Dhamira kuu ya mwanafasihi katika utanzu wowote ule wa fasihi huwa kuyatumia maandishi au simulizi kwa ajili ya kuwalea, kukuza hadhira yake kwenye misingi inayokubalika, na kuijenga jamii mpya iliyokitwa kwenye

maadili na falsafa njema ya maisha (Wamitila, 2003). Jambo hili pia linasisitizwa na Ndungo (1985) anayesema kwamba fasihi ni kielelezo cha hali halisi ya maisha. Kulingana na Ndungo, mwandishi kama tu mwanajamii mwingine yeyote, huandika au kusimulia yale anayoona katika jamii yake.

Mabadiliko katika jamii huwachochea watunzi kutunga nyimbo zinazoendana na wakati. Njogu na Chimerah (1999) wanasema kuwa kuna uhusiano mkubwa kati ya sanaa na matukio ya kijamii; kwa hivyo, msanii hawezi kujitenga na matukio ya jamii yake kwani ana masilahi katika jamii hiyo. Maelezo haya yanamaanisha kwamba maudhui ya msanii hutokana na mambo ambayo yanamsukuma kwa kipindi alicho nacho. Nyimbo anuwai za jando za Wakamba zinabeba dhima nyingi kama tunavyoona katika sehemu ifuatayo.

**4.1 Kubainisha Umuhimu wa Elimu**

Baada ya majilio ya wakoloni, jamii ya Wakamba sawa na jamii nyingi za Kiafrika, ilifuata elimu ya Kimagharibi ambayo ilihusu usomaji wa darasani. Suala la elimu ya Kimagharibi ni nyeti katika jamii ya kisasa kwa sababu inahusishwa na nguvu na uwezo wa kiuchumi (Kaui, 2008). Kutokana na imani hii, baadhi ya nyimbo za jando za Wakamba zinasisitiza maudhui ya umuhimu wa elimu katika kubadilisha maisha ya wanajamii kiuchumi. Lengo la kutungwa kwa nyimbo hizi ni kuhimiza vijana watilie maanani umuhimu wa masomo, ili wabadilishe maisha yao. Aidha, zinachochea wanajamii wawaelimishe watoto wao. Mfano ni wimbo ufuatao wa "Syokimau":

| | |
|---|---|
| *Syokimau ndathanie* | Syokimau alitabiri |
| *Kukooka kisomo kya Mungelesa* | Kutakuja masomo ya Mwingereza |
| *Kwatai kisomo* | Shikilieni masomo |
| *Muikekye muthanga* | Msije kutupa mchanga |

Wimbo huu huimbwa ili kuwahimiza watahiriwa na vijana wengine watilie maanani elimu kama vile mshororo wa 3 unavyosema kwatai kisomo (shikeni masomo). Kulingana na wimbo huu, wanapaswa kujiepusha na kazi za sulubu ambazo hazina mapato mazuri ikilinganishwa na masomo.

Lugha ya kitamathali iliyotumika katika wimbo huu imechota maudhui yake kutoka katika mazingira ambayo wazungumzaji wa lugha husika huishi. Wakamba ni wakulima. Wanapanda mahindi, maharagwe na mtama, miongoni mwa mazao mengine. Wao huchimba milevu (mitaro) shambani ili kuzuia mchanga kubebwa na maji ya mvua. Uchimbaji wa mitaro hii si kazi rahisi bali ni ya sulubu inayohitaji muda na nguvu nyingi, na huchimbwa na wanaume kwa malipo fulani. Kwa hivyo, msanii anawahimiza vijana wasome wasije kuchimba mitaro ambayo huchimbwa na walalahoi ambao hawana njia nyingine ya kujitafutia riziki. Kuuelewa utamaduni wa

jamii husika kunafanikisha ujumbe unaoibuliwa na wimbo wa "Syokimau" kwa walengwa wake.

**4.2 Kutoa Tahadhari Dhidi ya UKIMWI**

Kwa mujibu wa Ngoyani (2006) na Kinara (2012), maradhi ya UKIMWI yaligundulika Afrika Mashariki mwaka 1980. Ugunduzi wa maradhi haya ulileta wasiwasi na kuzifanya serikali za Afrika Mashariki na wanajamii kuyumbayumba kabla ya kupata uelewa wake kamili. Ngoyani (2006) na Kinara (2012) wanasema kwamba maradhi ya UKIMWI, mwanzoni wa mwaka wa 1980, yalijulikana kwa majina mengi ambayo yalitokea kule Marekani ambako ndiko inasemekana ugonjwa huo ulianzia. Baadhi ya majina haya ni kama Gay cancer, wrath of God syndrome miongoni mwa majina mengine. Humu nchini Kenya, maradhi haya yalijulikana kama UKIMWI ikiwa na maana ya Upungufu wa Kinga Mwilini ambapo mwili hupoteza kinga dhidi ya magonjwa na kusababisha kushambuliwa na magonjwa nyemelezi.

Mutembei (2009) na Kinara (2012) wanasema kwamba maradhi haya yalitambuliwa kwanza nchini Kenya miongoni mwa wanajamii walioishi katika makao duni na waliojishughulisha na uvuvi na biashara ndogondogo. Utambuzi huu uliwapa wanajamii nafasi ya kuubatiza majina tofauti kama vile 'maradhi ya wafanyabiashara', 'maradhi ya makahaba', na 'maradhi ya madereva wa masafa marefu' ambao walikuwa wakifanya biashara ya usafirishaji wa bidhaa kati za nchi ya Kenya, Uganda na Tanzania.

Tangu UKIMWI ulipogunduliwa nchini Kenya katika miaka ya 1980, jamii imeendelea kuhamasishwa kuhusu namna ya kujikinga na kukabiliana na maradhi haya. Katika jamii ya Wakamba, nyimbo za kisasa za jando hutungwa ili kuwatahadharisha wanajamii hasa vijana kuhusiana na maradhi haya hususani wimbo wa "Waminwa ni Katulilangi" (Ukimalizwa na Katulilangi). Tazama ubeti ufuatao wa wimbo huo:

| | |
|---|---|
| *Waminwa ni nzou, ndikautula muti* | Ukimalizwa na ndovu , sitakulaumu |
| *Waminwa ni nzoka, ndikautula muti* | Ukimalizwa na nyoka, sitakulaumu |
| *Waminwa ni muthesu, ndikautula muti* | Ukimalizwa na donda ndugu, sitakulaumu |
| *Waminwa ni kitundumo, ndikautula muti* | Ukimalizwa na radi, sitakulaumu |
| *Indi waminwa ni muthelo, ngautula muti* | Lakini ukimalizwa na Ukimwi, nitakulaumu |
| *Waminwa ni Katulilangi, ngautula muti* | Ukimalizwa na Katulilangi, nitakulaumu. |

Katika wimbo huu, neno waminwa (ukimalizwa) limebeba ujumbe wa msanii kwa watahiriwa na wanajamii kwamba kifo kinaweza kutokea kupitia njia nyingi. Kwa mfano, binadamu anaweza kufariki kutokana na kuuliwa na ndovu, kuumwa na nyoka, kuuawa na donda ndugu, na kupigwa na radi. Hata hivyo, kumalizwa na UKIMWI kupitia kwa kuambukizwa na wanawake kama Katulilangi kunalaumiwa

katika jamii ya Wakamba kama inavyodhihirika katika mshororo wa 5 na 6 wa wimbo huu. Kwa mujibu wa wimbo huu, Katulilangi ni mwanamke ambaye hana msimamo. Amepewa jina la kimajazi kutulilanga likiwa na maana ya 'kurukaruka'. Anashiriki ngono na wanaume wengi. Hivyo, wanaume wanatahadharishwa dhidi ya kujihusisha na wanawake kama hawa ili kujiepusha na ugonjwa wa UKIMWI.

**4.3 Kujenga Ushirikiano wa Kijamii**

Maudhui ya ushirikiano wa kijamii yanapatikana katika kipindi cha kabla na baada ya ukoloni. Jinsi asemavyo Mbiti (1969), hii inatokana na sababu kwamba jamii ya Wakamba inaamini katika ukweli uliomo katika methali, 'umoja ni nguvu na utengano ni udhaifu.' Jamii ya Wakamba iliishi kwa ushirika na umoja kabla ya majilio ya wakoloni. Mbiti (keshatajwa) anabainisha utamaduni wa Wakamba wa kushirikiana anapoeleza kwamba, katika jamii hii, kila mtu aliishi kwa ajili ya mwingine. Ushirika huu uliwapa wanajamii mshikamano ambao uliwawezesha kukabiliana na baadhi ya matatizo kama jamii moja. Kupitia desturi hii, nyimbo za jando za kisasa hutungwa ili kuwahimiza wanajamii waendeleze ushirikiano wa kijamii. Mfano wa wimbo ambao unahimiza mshikamano huu ni "Muvuvi wa ndili" (Mpuliza baragumu). Tazama mishororo ifuatayo:

| | |
|---|---|
| *Muvuvi wa ndili ii* | Mpuliza baragumu ii |
| *Niwavuva ndili tweeyumilya* | Umepuliza baragumu tukajitokeza |
| *Twivoya ngwatanio Ukamba* | Twaomba ushirika Ukambani |
| *Twivoya Akamba makwatane mbau* | Twaomba Wakamba washirikiane |

Wimbo huu umesheheni maudhui ya ushirikiano wa wanajamii. Mtahiriwa anaambiwa katika mshororo wa pili kwamba niwavuva ndili tweeyumilya (umepuliza baragumu tukajitokeza). Kupuliza baragumu ni kujitangaza kwa mtahiriwa kwamba yuko tayari kutahiriwa na anaalika kila mwanajamii kushiriki katika sherehe yake ya kuingia utu uzima. Dhana ya upulizaji wa baragumu inaashiria uelewa wa kila mtahiriwa kwamba jamii nzima ya Wakamba ni muhimu kwake na anapaswa kualika kila mwanajamii katika siku hii muhimu. Kila mwanajamii alitarajiwa kuhudhuria sherehe hii kwa sababu ilikuwa ya jamii nzima. Dhima ya ushirikiano inatilia umuhimu na wimbo huu wa "Muvuvi wa ndili" ambao ungali unaimbwa katika jamii ya Wakamba ya kisasa. Lengo la wimbo huu kwa jamii ya sasa ni kusisitiza kwamba, wanajamii wanatarajiwa kuishi pamoja kwa ushirika kama vile jamii ya jadi ya Wakamba ilivyoishi. Maneno 'Kushikana mbavu' katika mshororo wa nne yametumiwa kitamathali. 'Kushikana mbavu' kwa mujibu wa wimbo huu, ni kushirikiana. Ni ishara ya kuishi pamoja kwa kutegemeana.

**4.4 Kukashifu Maadili Ajinabi**

Baadhi ya nyimbo katika kipindi cha baada ya ukoloni zinawaelimisha watahiriwa kuhusu umuhimu wa maadili ambayo jamii inawatarajia kushikilia. Baadhi ya nyimbo zimetungwa ili kuwamulikia vijana wa kiume na wa kike kuhusu tabia za

kuajabia, mathalani, ushoga na ndoa za jinsi moja. Katika jamii ya jadi ya Wakamba, mvulana alichaguliwa mke na baba ama mjomba. Vijana, kote duniani, sasa wana utamaduni wao ambao Brake (1980) anaueleza kama 'ulimwengu huru' wa vijana ulio na mitindo na njia za maisha ambazo vijana hufuata ili kujitofautisha na utamaduni wa wazazi wao. Utamaduni wa vijana kwa kiasi kikubwa ni zao la maendeleo katika jamii za ulimwengu.

Kadiri jamii inavyosonga mbele kimaendeleo, ndivyo ambavyo utamaduni wa vijana unakuzwa, unaimarishwa na kusambazwa miongoni mwa vijana kote duniani. Vijana wamebuni utamaduni wao kama njia moja ya kuasi utamaduni uliotawaliwa na wazee. Wanataka kujihusisha na tabia kama vile matumizi ya dawa za kulevya, ushoga, uasi wa maadili ya kijamii, mitindo mipya ya mavazi, na muziki, tabia ambazo huwatenga wazee. Kulingana na Kaplan (1989), hili ni jaribio la vijana kupania kuonesha nguvu na uwezo wao wa kijamii. Ujumbe wanaopitisha ni kuwa hawako tayari kushiriki utamaduni unaowadhibiti na kuwanyima nafasi yao katika jamii. Ili kuwaonya vijana kuhusiana na tabia ya ushoga, nyimbo za jando zimetungwa kukashifu tendo hili. Wimbo wa "Kiwanza kila kinai Kamuvalu" (Uwanja uliokuwa Kamuvalu) ni mfano mzuri. Tazama:

| | |
|---|---|
| *Kiwanza kila kinai Kamuvalu* | Uwanja uliokuwa Kamuvalu |
| *Mwikuyu niwakindana na Mukamba* | Mkikuyu amefanya ngono na Mkamba |
| *Ko nzau ikindanaa na ingi?* | Kwani dume hushiriki ngono na mwingine |

Wimbo huu huimbwa katika jando za kisasa ukiwa na lengo la kuwahamasisha watahiriwa kuhusu athari za mabadiliko ya maisha. Ulitungwa ili kuwatahadharisha vijana kujiambaa na ubasha. Mtunzi wa wimbo huu anaonesha kuajabia kitendo hiki kama vile mshororo wa 3 unavyouliza, 'kwani dume hufanya ngono na mwingine?' Msanii anatumia maswali ya balagha ili kusisitiza na kuchochea hisia na ari kuhusu suala la ubasha. Katika utamaduni asili wa Kiafrika, tabia kama hii haikuwapo, na kama ilikuwapo, ilifanyika kwa siri sana kwa sababu tabia yoyote ambayo ilienda kinyume na maadili ya kijamii ilipigwa vita.

Katika jamii ya jadi ya Wakamba, mwanamume alitarajiwa kuoa mwanamke ili wazae watoto wa kuendeleza ukoo wake na jamii nzima kwa ujumla. Wimbo huu "Kiwanza kila kinai Kamuvalu" umetumia tashbiha kwa kuwalinganisha wanaume na fahali katika mshororo wa 3 (kwani fahali hushiriki ngono na mwingine?). Fahali ana jukumu la kuzalisha mtamba lakini fahali na mwingine hawawezi kuzalisha. Kitendo cha fahali cha kujihusisha na ngono na fahali mwingine ni cha ajabu mno. Msanii anauliza swali hili la balagha kuonesha hisia zake za mchomo na mshangao ili kusisitiza kwamba, hakuna uwezekano wa fahali kutenda tendo la ngono na fahali mwingine.

Katika bara la Afrika, tabia ya ushoga inachukuliwa kama mwiko na inaenda kinyume na maadili ya Kiafrika (UN, 2005). Kwa mujibu wa Kaplan (1989) na Brake (1980), tabia ya ushoga baina ya vijana huigwa na kusambazwa kupitia TEHAMA. Njia za TEHAMA kama huduma za mtandao, setilaiti, runinga, na redio hutumika kuzalisha tamaduni mpya za vijana zinazojikita katika muziki, filamu, mavazi na mitindo ya maisha pamoja na bidhaa wanazotumia.

Nchini Kenya, tabia ya ushoga imeripotiwa baina ya vijana katika shule za mabweni. Vilevile, walio katika ndoa wameripotiwa kujihusisha katika ushoga nje ya ndoa zao (UN, 2005). Nchini Kenya, shirika la "The Gay and Lesbian Coalition of Kenya" liliundwa mwaka 2001 ili kupinga na kukashifu vitendo vya ushoga (Kaui, 2008). Shirika hili liliundwa kuwaelimisha wanajamii hasa vijana kuhusiana na athari za ushoga kama uambukizwaji wa magonjwa ya zinaa, ukiwamo UKIMWI. Aidha, utafiti kupitia shirika hili ulionesha kuwa mashoga hupata ugonjwa wa akili na wengi huwa wendawazimu (UN, 2005). Vijana Wakamba wanahimizwa kupitia nyimbo za jando kujitenga na ushoga kwani baada ya jando, jamii inawakubalia kuoa na kupata watoto watakaoendeleza jamii. Kuoa na kuzaa watoto ni jambo la msingi katika jamii ya Wakamba, hivyo, kila mwanamke na mwanamume waliofikia umri wa kuoa waliruhusiwa kufanya hivyo ili waweze kuendeleza ukoo wao.

Kwa mujibu wimbo wa "Kiwanza kila kinai Kamuvalu" (Uwanja uliokuwa Kamuvalu), kuporomoka kwa maadili ya vizazi vya kisasa kuna uhusiano mkubwa na kutupiliwa mbali kwa baadhi ya mila na tamaduni zilizotilia mkazo suala la maadili. Kulingana na wimbo huu, tabia ya mwanamume kutenda tendo la usenge na mwingine haikuwapo katika jamii ya jadi ya Mkamba aliyejulikana kama Mukamba wa w'o ama Mukamba kivindyo (Mkamba halisi).

**4.5 Umuhimu wa Kupanga Uzazi**

Jamii ya Wakamba hutumia nyimbo za tohara kuhimiza vijana kupanga uzazi ili kupata watoto wanaoweza kuwakimu. Nyimbo zinazohusiana na upangaji uzazi zinatokana na mabadiliko ya kijamii yaliyoletwa na elimu ya Kimagharibi ambayo ni ghali mno pamoja na njia mpya za uzalishaji mali. Kutokana na ugumu wa maisha, vijana wa leo wanahimizwa kupitia nyimbo, zikiwamo za jando, wapange uzazi ili wapate watoto wanaoweza kuwakimu vizuri. Miongoni mwa nyimbo zinazosheheni maudhui ya umuhimu wa kupanga uzazi ni wimbo wa "Makato mwiitu wa Masimba" (Makato msichana wa Masimba) ufuatao:

| | |
|---|---|
| *Makato mwiitu wa Masimba* | Makato msichana wa Masimba |
| *Vundisya muika kuumba* | Fundisha vijana kupanga uzazi |
| *Onakwa ngesila Tawa* | Hata mimi nilipitia Tawa |
| *Ngitonywa ndawa ya kuumba* | Nikadungwa dawa ya kupanga uzazi |

Wimbo huu huimbwa kwa lengo la kupitisha ujumbe kwa watahiriwa na vijana wengine kwamba, dunia ya leo imebadilika na wanahitajika kupata watoto ambao wanaweza kuwakimu kimaisha. Msanii anawahimiza vijana wafunzwe kupanga uzazi ili waweze kuzikimu familia zao.

**4.6 Kuangaza Majukumu ya Kiuana**

Baada ya majilio ya wakoloni, utamaduni wa Mwafrika uliathirika. Mabadiliko ya utamaduni yalianza baada ya elimu, dini na utamaduni wa Kimagharibi kupenya katika maeneo ya Ukambani katika miaka ya 1890 na 1900 (Kimilu,1962; Musyoka, 2012). Wamisionari walianza kuhubiri dhidi ya utamaduni wa Mwafrika kwa ujumla. Mila kuhusu majukumu ya kiuana ikaanza kupata athari ya mahubiri haya pamoja na athari za uchumi wa pesa uliobadilisha njia za uzalishaji mali. Wanajamii wasomi waliohama kijijini na kwenda kuishi katika miji mikuu kutokana na sababu za kikazi ndio walioathirika zaidi na utamaduni wa kigeni.

Kutokana na athari za utamaduni wa Kimagharibi, baadhi ya Wakamba walikengeushwa na kutengwa na jamii yao ya jadi ambayo ilikuwa na mipaka kuhusu majukumu ya wanaume na wanawake. Kutokana na tabia ya mwanamume kuanza kutekeleza majukumu ya kike, wasanii nao wamelivalia njuga suala hili na kutunga nyimbo zinazoonesha madhara ya ukengeushi huu. Aidha, wanatunga nyimbo kukashifu wanaoenda kinyume na utamaduni wao wa jadi kuhusu majukumu ya kiuana. Wimbo ufuatao wa Ninoonie kindu kyanzenya (Niliyoyaona yalinishangaza) ni mfano mzuri wa unaokashifu ukengeufu huo.

| | |
|---|---|
| *Ninoonie kindu kyanzenya* | Niliyoyaona yalinishangaza |
| *Mungelesa aetie kiumo nduani* | Mwingereza ameleta laana kijijini |
| *Aume nimavulaniilwe* | Wanaume wamechanganyikiwa |
| *Masyokie ikoni* | Wamerudi jikoni |
| *Masyokie usini* | Wamerudi mtoni |
| *Indo ikaithwa nuu?* | Mifugo itachungwa na nani? |

Wimbo huu uliimbwa kwa njia ya kejeli. Ni wimbo ambao unakashifu na kusimanga utamaduni wa Mwingereza ambao hauna mipaka kati ya majukumu ya kiuana, na ambao baadhi ya wanaume hasa wasomi wamekengeushwa nao. Katika mshororo wa 2, msanii anasema ‘Mwingereza ameleta laana kijijini.’ Laana kwa mujibu wa wimbo huu ni kutelekeza utamaduni wa Wakamba na kupapia utamaduni wa kigeni. Kulingana na wimbo huu, wanaume wameanza kutekeleza majukumu ya kike kama vile mshororo wa 3 na wa 4 inavyoshikilia, ‘wanaenda jikoni na mtoni’. Kulingana na msanii, kuenda jikoni na mtoni kuna maana ya kupika na kuchota maji, majukumu ambayo yametengwa kwa ajili ya mwanamke katika jamii ya jadi ya Wakamba. Lengo la wimbo huu ni kukashifu utamaduni wa Kimagharibi ambao umeondoa mipaka kati ya mwanamke na mwanamume kupitia majukumu wanayotarajiwa na

jamii kuyatekeleza. Unasimanga wanaume ambao wamebadilishana majukumu yao na mwanamke.

Katika jamii za Kiafrika, kuna uhusiano mkubwa wa uana na majukumu ambayo binadamu hutengewa na jamii. Umuhimu wa kila jinsia kutekeleza majukumu yake umemsababisha msanii kuuliza swali la balagha "mifugo itachungwa na nani?" (mshororo wa 6), iwapo wavulana wamegeukia majukumu ya kike. Kulingana na wimbo huu, kupapia utamaduni wa Wazungu kunawadhalilisha wanaume wa Kiafrika kwa kuwakengeusha kiasi cha kutekeleza majukumu ambayo yametengewa wanawake. Mtunzi wa wimbo huu anaona tabia ya mwanamume kutekeleza majukumu ya kike kama jambo la ajabu. Anasema ninoonie kindu kyanzenya (niliyoyaona yalinishangaza) katika mshororo wa 1.

Kimilu (1962) anaeleza kuwa katika jamii ya jadi ya Wakamba, Mukamba wa w'o (Mkamba halisi) ni yule aliyefuata mila na utamaduni wa jamii yake. Mwanamume halisi katika jamii hii alitengewa majukumu mahususi kama vile kuchunga mifugo, kuilinda jamii, na kuikimu familia yake. Wanawake nao walitengewa majukumu kama vile kuzaa, kuwalea watoto, kuwapikia, kuchota maji, kutafuta kuni, kulima, kupalilia, na kuvuna mazao. Wimbo huu unatoa rai kwa watahiriwa washike mila na tamaduni zao ili waondoe laana katika jamii.

### 4.7 Kuangaza Changamoto katika Ndoa za Kisasa

Suala la ndoa ni kipengele kinachotambuliwa duniani kote kama suala nyeti lenye kuathiri maendeleo ya kijamii (Mbiti, 1991). Suala la matatizo katika ndoa za kisasa limewavutia wasomi katika nyanja mbalimbali kama vile dini, historia, saikolojia, isimujamii, filosofia na fasihi (Simiyu, 2007). Wasanii wa nyimbo za jando za Wakamba wamelivalia njuga suala la ndoa, kwa mfano, kupitia wimbo "Mbulwa" (Mbulwa). Wimbo huu unawatahadharisha wavulana hatari iliyopo ya kuchagua wanawake wasiowajua mienendo yao vizuri:

| | |
|---|---|
| *Mwana wa mwendya niki wambikisye iko* | Binamu kwa nini ulinitupa motoni |
| *Uimbonania na Mbulwa mwiitu wi* | Ukanionesha Mbulwa msichana aliye na |
| *Mavenzi movungu* | Mapenzi ya uongo |
| *Nikilya noosa musaala mwisowa mwai* | Nikichukua pesa mwishoni mwa mwezi |
| *Aimbonethya tuthi tukakunde twiili* | Ananiambia twende tukanywe mbili |

Katika wimbo huu, msanii anasema mwanamke aliyetambulishwa kwake aitwaye Mbulwa ana mapenzi ya uongo kama mshororo wa 2 na wa 3 unavyothibitisha; 'Ukanionesha Mbulwa msichana mwenye mapenzi ya uongo' (Uimbonanya na Mbulwa mwiitu wi mavenzi movungu). Licha ya kuwa na mapenzi ya uongo, Mbulwa anasawiriwa kama mlevi katika mshororo wa 2. Anasema, 'kila mwisho wa mwezi anamwambia waende wakanywe mbili'. Hii ni tabia nyingine ambayo

inamfanya mhusika kulalamikia tabia ya mkewe, Mbulwa. Vilevile, Mbulwa ni mchawi. Haya yanabainishwa kupitia sehemu ifuatayo ya wimbo huu:

| | |
|---|---|
| *Navindukie neethia mbulwa e muthei* | Niliamka nikamkuta akiwa uchi |
| *Aithyululuka ngua syakwa ailuma ta simba* | Akizunguka nguo zangu akinguruma kama simba |

Kulingana na msanii wa wimbo huu, tabia ya Mbulwa ya kuvua nguo usiku na kumzunguka mumewe huku akinguruma kama simba ni ya kichawi. Uchawi ni miongoni mwa imani ambazo zimekita mizizi katika jamii ya Wakamba. Jamii hii inaamini kwamba, kuna wanajamii ambao ni wachawi na huwadhuru wengine kwa kuwaroga. Miongoni mwa athari za uchawi ni mtu kuzugwa akili mpaka anasahau majukumu yake ya kimsingi kama kuwakimu wazazi na jamaa zake. Katika wimbo huu, mhusika anasema kwamba haendi kwao na anafikiria Mbulwa 'alimuendea' katika mshororo wa 6. Neno 'kumuendea' limetumiwa kimafumbo katika wimbo huu. Lina maana ya 'kurogwa'. Matumizi ya maneno kulingana na muktadha ili kuibua mawasiliano yanayotarajiwa yanaungwa mkono na Hymes (1974) anaposema kuwa, ili kuelewa maana ya misemo na utaratibu wa kuongea, ni lazima suala la muktadha lizingatiwe.

Wimbo huu huimbwa ukiwa na lengo la kukashifu unafiki wa wanawake walio katika ndoa na ambao wana tabia hasi kama ya mwanamke anayeitwa Mbulwa katika wimbo huu. Dhima moja kuu ambayo hutekelezwa na nyimbo za jando ni ile ya kuwapiga vita wale wanaoenda kinyume na maadili ya kijamii. Katika jamii ya jadi ya Wakamba, msichana akivunja ungo alikuwa anapitishwa katika unyago ili kuashiria kwamba, amevuka kutoka awamu ya utotoni hadi utu uzima. Sherehe ya unyago ilikuwa muhimu katika jamii ya Wakamba kwa sababu, licha ya msichana kupewa hadhi mpya yenye matarajio, matakwa na majukumu mapya baada ya kutahiriwa, alipitishwa kwenye mafunzo makali kuhusiana na mambo ya unyumba na namna ya kumtunza mume.

Katika jando za kisasa, wimbo huu huimbwa ukiwa na lengo la kuwatahadharisha vijana dhidi ya wanawake wasio na maadili kulingana na utamaduni wa Wakamba. Katika muktadha wa wimbo huu, Mbulwa ni taswira ambayo inawakilisha wanawake wote wa kisasa ambao wameasi tamaduni zao kutokana na kukengeushwa na tamaduni za kigeni. Mwanamke, kulingana na utamaduni wa Wakamba, anapaswa kushikilia majukumu yake ya kiuana kama vile kuzaa, kulea watoto, na kumtunza mumewe. Hapaswi kuenda kwa vilabu kushiriki vileo kama wanaume.

Msanii ametumia mbinu ya istiara kumlinganisha Mbulwa na moto. Katika mshororo wa 1, msanii anasema 'binamu kwa nini ulinitupa motoni?' Kumuoa Mbulwa, kwa mujibu wa wimbo huu, ni sawa na kumtumbukiza mhusika katika moto. Nyimbo za jando za kisasa pia husawiri suala la ugomvi katika ndoa. Ugomvi katika ndoa za kisasa limekuwa suala nyeti katika ulimwengu wa leo. Wasanii wa nyimbo za jando za Wakamba nao wamelivalia njuga suala hilo ili kusheheni falsafa, imani na mtazamo wa jamii ya Wakamba.

**5.0 Hitimisho**

Makala haya yameonesha kwamba jamii ya Wakamba inatilia mkazo tohara kwani ni kivuko kwa wavulana kutoka maisha ya utotoni hadi utu uzima. Tohara huwapa vijana wa kiume mafunzo ambayo ni adimu kupatikana katika miktadha mingine ya kijamii. Haya yanajumuisha mafunzo kuhusu unyumba, umuhimu kuhusu elimu mpya ya kisasa, majukumu ya uana, ndoa za kisasa, uzazi wa mpango, siri na historia ya jamii. Hivyo, makala haya yameeleza umuhimu wa nyimbo za kisasa za jando kwa vijana katika jamii ya Wakamba katika karne ya ishirini na moja.

**Marejeleo**

Brake, M. (1980) The Society of Youth Culture and Youth Subcultures: Sex, Drugs and Rock 'n' Roll? London: Routledge and Kegan Paul.

Finnegan, R. (1977) *Oral Traditions and Verbal Arts: Guide to Research*. London: Routledge.

Hymes, D. (1974) *Foundations in Social Linguistics An Ethnographic Approach*. Philadelphia: University of Pennsylvania Press.

Kaplan, E.A (1989) *Rocking Around the Clock: Music, Television. Postmodenism and Consumer Culture*. London: Mathuen.

Kaui, M. (2008). *Usawiri wa Vijana katika Tamthilia teule za Kiswahili*. Tasnifu ya Uzamili (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Kieti, M. (1999) *Myali songs. Social Critique among the Kamba*. Tasnifu ya Uzamili. (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Nairobi, Nairobi.

Kieti, M. na Coughlin, P. (1990) *Barking, U Will Be Eaten! The Wisdom of Kamba Oral Literature*. Nairobi: Phoenix Publishers.

King'ei K. (1982) *Uhakiki wa Nthimo(Methali) za Kikamba kwa kufatisha misingi ya methali za Kiswahili*. Tasnifu ya Umahiri. Chuo Kikuu cha Nairobi, Nairobi.

Kinara, G. (2012) *Maudhui ya Ukimwi katika Ua la Faraja na Kala Tufaha*. Tasnifu ya Uzamili (Haijachapishwa. Chuo Kikuu cha Kenyatta, Nairobi.

Kimilu, D. (1962) *Mukamba wa w'o*. Nairobi: East Africa Literature Bureau.

Kyavu P.N (1980) *Traditional Musical Instruments of Kenya*. Nairobi: Kenya Literature Bureau.

Mbiti, J.S. (1969) *African Religion and Philosophy*. Nairobi: East African Educational Publishers.

Mutembei, A.K. (2009) *Ukimwi katika Fasihi ya Kiswahili 1982-2009*. Dar es Salaam: Taasisi ya Taaluma za Kiswahili.

Nandwa, J & Bukenya, A (1983) *African Oral Literature for Schools*. Nairobi : Longman.

Ndeti, K. (1972) *Elements of Akamba Life*. Nairobi: East African Educational Publishers.

Ngara E. (1982) *Stylistic Cricism and the African Novel*. Nondon: Heinemann.

Ndungo, C. (1985) *Wanawake na Mabadiliko ya Kihistoria Katika Fasihi ya Kiswahili*. Tasnifu ya Uzamili (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Kenyatta, Nairobi.

Njogu, K. na Chimera, R. (1999) *Ufundishaji wa Fasihi. Nadharia na Mbinu*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Ngoyani, D.S. (2006) "Lexical Innovation in Tanzania's Political Discourse." Kiswahili. Juz. 69: 13-19.

Ntarangwi, G.M. (2004) *Uhakiki wa Kazi za Fasihi*. Augustana College: Rock Island.

Nzioki, S. (1982) *People of Kenya. The Akamba*. Nairobi: Evans Brothers.

Senkoro, F.E.M.K. (1987) *Fasihi na Jamii*. Dar es salaam: Press and Publicity Centre.

Simiyu, F.W. (2007) *Nyiso za Wabukusu, Maudhui na Lugha*. Tasnifu ya Uzamili (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Kenyatta, Nairobi.

Somba, J.N. (1972) *Elements of Kamba Life*. Nairobi: East African Educational Publishers.

Wanyama, M.N. (2005) *Ujumi katika Muziki wa Kiafrika: Mfano wa Muziki wa Tohara ya Wabukusu*. Tasnifu ya Uzamili (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Moi, Eldoret.

Wathome, R. (2009) *Mtindo katika Nyimbo za Jamii ya Wakamba wa Masaku ya Kati*.Tasnifu ya Uzamili (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Kenyatta, Nairobi.

Watuma, B. (2001) *Mukamba na Syithio syake*. Nairobi: Sengani Publishers.

Wamitila, K.W. (2003) *Kichocheo cha Fasihi Simulizi na Andishi*. Nairobi: Phoenix Publishers.